# SHIRIKISHO LA MAREKANI WIZARA YA ELIMU

## Idara ya Haki za Kiraia (Office of Civil Rights) (OCR)
## Fomu kwa ajili ya Malalamiko dhidi ya Ubaguzi

**1. Andika maelezo yakuhusuyo.**

Jina la Kwanza: ________________ Jina la Ubini: ________________________________

Anwani: ____________________________________________________________

Mji: ____________________ Taifa: _______________________ Ishara ya Siri: __________________

Nambari ya Simu—Mchana: ________________________ Magharibi: __________________________

Muda bora wa kukupigia Simu: ____________________________________________

Anwani yako ya barua pepe: ______________________________________________

**2. Nani mwengine twaweza kumpigia Simu pindi tutashindwa kukupata?**

Jina la mhusika: ____________________________ Uhusiano nawe: ____________________________

Nambari ya Simu Mchana: ________________________________________________

**3. Nani aliye fanyiwa kisa cha ubaguzi? Andika maelezo yote iwezekanavyo.**

☐ Wewe binafsi ☐ Mtu mwengine

Iwapo ni mtu mungine siyo wewe binafsi, tafadhali eleza:

Jina la Mhusika: ____________________________________________________

Nambari ya Simu—Mchana: ________________________ Magharibi: __________________________

Uhusiano nawe: (k.m. mvulana au msichana wako) ________________________________

Anwani ya Mhusika, **iwapo ni tofauti na yako:** ______________________________

Mji: ____________________ Taifa: _______________________ Ishara ya Siri: __________________

*Iwapo aliye fanyiwa kisa cha ubaguzi ana umri wa myaka 18 au ni mtu mzima, tutahitajisahihi ya mtu huyo kabla ya kujihusisha na malalamiko haya. Iwapo mhusika ni mtoto na hauna mamlaka ya kisheria ya kufanya utetezi kwa niaba yake inahitajika, sahihi ya mzazi au mlezi wake.*

**4. Je, ni taasisi gani iliyo husika na ubaguzi?**
(Sheria za OCR zinahusika na sekta ya elimu, taasisi kama shule za wilaya, Koleji na vyuo vikuu, maktaba za umma na katika taasisi za kikazi)

Jina la Shirika: ____________________________________________________

Anwani: ____________________________________________________________

Mji: ____________ Taifa: ____________ Ishara ya Siri: ____________

Shule au Idara iliyo husika: ____________________________

**Je, ulijaribu kutatua malalamiko yako kupitia utaratibu wa taasisi ya manung'uniko, kwa kusikilizwa au kupitia taasisi nyingine yoyote ile?**

☐ Ndiyo ☐ Hapana

**Iwapo ndiyo, fanya maelelezo yafuatayo:**

Jina la Shirika: ____________________ Tarehe ya malalamiko: ____________

Sababu ya malalamiko:

________________________________________

________________________________________

________________________________________

(Iwapo una maelezo zaidi, tafadhali andika kwenye karatasi nyingine.)

**5. Eleza kisa cha ubaguzi.**

Ni marufuku kwa mujbu wa OCR kufanya ubaguzi kwa misingi ya kabila, rangi, asili ya mtu, jinsia, ulemavu, na/au umri.

Ni kwa misingi gani ulifanyiwa kisa cha ubaguzi? (Waweza kuelezaidi ya sababu moja)

☐ kabila au rangi ☐ asili yako ☐ ulemavu ☐ jinsia ☐ umri
☐ uhusiano sababu ulilalamika au ulidai haki zako

Katika nafasi uliyo pewa hapa chini, tafadhali eleza kila kisa cha ubaguzi kwa uchambuzi. Kwa kila kisa, unahitaji kufanya maelezo yafuatayo:

- tarehe kilipo tokea kisa cha ubaguzi;
- jina (majina) la aliye fanya ubaguzi;
- ilikuwaje;
- mashahidi (iwapo kuna yeyote);
- kwanini una itikadi kuwa ulifanyiwa ubaguzi, je ni kwa sababu ya [kabila, jinsia, ulemavu, au ni kwa misingi yoyote ile uliyo eleza hapo juu] au kwanini una itikadi kuwa kisa hicho kilikuwa cha kisasi.

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

(Iwapo una maelezo zaidi, tumia karatasi nyingine)

**Je, unadhani umeandika maelezo yanayo weza kutusaidia kuelewa malalamiko yako?**

☐ Ndiyo ☐ Hapana

Utapewa muongozo ili ukabidhi maelezo yako **(tafadhali usikabidhi hati sahihi).**

**6. Malalamiko yako yapasa kukabidhiwa katika muda wa siku 180 tangu kimetokea kisa cha ubaguzi.**

*Sheria dhidi ya ubaguzi zina agiza kuwa malalamiko dhidi ya ubaguzi yapasa kuwa yamewasilishwa katika afisi zetu mnamo muda wa siku 180 tangu yamekuwepo madai ya tukio la ubaguzi Iwapo madai ya tukio la ubaguzi yametokea katika muda wa zaidi ya siku 180 kabla ya muhuri wa posta au tarehe ya stkabadhi ya malalamiko, waweza kuomba kusamehewa sababu ya kuwa muda wa kisheriawa siku 180 umepita.*

Andika tarehe kilipo tokea kisa cha mwisho cha ubaguzi: ____________________

Je, unaomba kusamehewa sheria ya muda wa mwisho wa siku 180 kutokana na kutowasilisha malalamiko yako dhidi ya kisa cha ubaguzi kilicho tokea katika muda wa zaidi ya siku 180 kupita?

☐ Ndiyo ☐ Hapana

Eleza hapa chini sababu hukuwasilisha malalamiko yako kabla ya siku 180:

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

(Iwapo una maelezo zaidi, tumia karatasi nyingine.)

**7. Je, ungelipendelea taasisi ikusaidiye nini katika malalamiko yako? Je, unapendekeza jawabu gani?**

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

(Iwapo una maelezo zaidi, tumia karatasi nyingine.)

**8. Tafadhali soma Fomu za utaratibu wa Kuridhia na Maelezo kuhusiana na malalamiko ya OCR. Kabla ya kukamilisha utaratibu wa msingi wa malalamiko yako, unapasa kusaini malalamiko yako na Fomu ya Kuridhia inayo turuhusu kushughulikia chochote kile. Tilia sahihi fomu iliyo hapa chini, weka tarehe na uitume kupitia afisi rasmi za kisheria.**

| | |
|---|---|
| ______________________________ | ____________________ |
| (Sahihi) | (Tarehe) |

# *Idara ya Haki za Kiraia na Fomu za Kuridhia*

***Idara ya Haki za Kiraia na Fomu za Kuridhia***

## Tafadhali tia sahihi, na tarehe kwenye fungu A au fungu B:

Jina lako kwa Herufi Kubwa: ________________________________

Taasisi inayo lalamikiwa: ________________________________

**A.** Nimesoma **Taarifa kuhusu Uchunguzi wa Maelezo ya Kibinafsi**. Kama mlalamikaji, Mimi naelewa kuwa kipindi cha uchunguzi OCR yaweza kuwa ilikuta ni muhimu mimi kujitambulisha kwa maafisa wa taasisi inayo chunguzwa  Nakubaliana na hilo. Na naelewa pia kuwa chini ya sheria za Uhuru wa Maelezo, OCR ingelinitaka nijieleze kwa misingi ya uchunguzi huu, licha tu kwa sababu maalumu, kama chini ya haki ya mtu kutoingiliwa.

________________________ ________________
(Sahihi) (Tarehe)

AU

**B.** Ningelipendelea kuwasilisha malalamiko haya, lakini bila ya mimi kuridhia kutoa maelezo binafsi. Nimesoma Taarifa kuhusiana na Uchunguzi wa Maelezo yangu Binafsi na naelewa kuwa OCR yaweza kufunga jalada la malalamiko haya, iwapo OCR haiwezi kuendelea na utaratibu wa uchunguzi bila ya mimi kujieleza na kujitambulisha.

________________________ ________________
(Sahihi) (Tarehe)

## *Idara ya Haki za Kiraia*

**Taarifa kuhusiana na Uchunguzi wa Maelezo Binafsi**

Ili kutatua malalamiko yako, OCR yaweza kuhitaji kukusanya uchambuzi wa maelezo binafsi, mathalani shughuli zako kama mwanafunzi au kama mfanyakazi. Hakuna sheria inayo kushurutisha kufanya maelezo binafsi kwa OCR na wala hakuna vikwazo walalamikaji wanavyo weza kuchukuliwa au mtu yeyote asiye taka kutoa ushirikiano katika fani ya maelezo binafsi kipindi cha utaratibu wa kutafuta utatuzi wa malalamiko. Hatahivyo, iwapo OCR haiwezi kupata maeelezo inayo hitaji ili kutatua malalamiko yako, itawajibika kufunga jalada la malalamiko yako.

Sheria ya mtu kutoingiliwa ya 1974 (Privacy Act of 1974), 5 U.S.C. § 552a, na Sheria ya Uhuru wa Maelezo (Freedom of Information Act) (FOIA), 5 U.S.C. § 552, muongozo wa maelezo binafsi zilizo pewa taasisi zote za Shirikisho ikiwemo OCR.

Sheria ya Kutoingiliwa ya 1974 inalinda maelezo ya watu kutotumiwa kiholela katika maelezo binafsi yaliyo mikononi mwa serikali ya Shirikisho. Hayo yanatekelezwa sambamba na rekodi za shughuli za mtu zinazo hifadhiwa na serikali ya Shirikisho na maelezo ya mtu huweza kupatikana kwa jina la mtu, kutoka taasisi ya akiba ya uzeeni au katika sehemu nyingine zinako hifadhiwa rekodi za watu. Kuna utaratibu wa jinsi ya kuweza kupata maelezo binafsi ya mtu, jinsi yanavyo hifadhiwa, jinsi ya kuyatumia, na jinsi ya kuwapelekea maelezo hayo maafisa wa taasisi nyingine za serikali ya Shirikisho.

Maelezo yaliyo kusanywa na OCR hufanyiwa uchambuzi na afisa wa taasisi aliye ruhusiwa na uchambuzi huo utatumiwa tu katika misingi ya haki za kiraia mnamo utekelezaji sheria. Hatahivyo, kwa minajili ya kutatua malalamiko OCR inaweza kuhitaji kuweka bayana baadhi ya maelezo kwa watu wasio kuwa wa taasisi kwa ajili ya ukaguzi au kwa ajili ya kuongeza baadhi ya maelezo, kama vile umri, au hali ya kiafya ya mlalamikaji. Kadhalika, OCR inaweza kuombwa iweke bayana maelezo chini ya FOIA (jadili hapo chini). OCR haiwezi kutangaza maelezo binafsi ya mtu kwenye taasisi yoyote ile au kwa yeyote licha tu katika moja juu ya sababu 11 zinazo elezwa na sheria ya Wizara 34 C.F.R. § 5b.9(b).

OCR kamwe haitangazi jina au utambulisho mungine wa mtu ila iwapo ni muhimu kwa ajili ya kukamilisha uchunguzi au kwa ajili ya utaratibu wa kisheria dhidi ya taasisi iliyo kiuka sheria, au endapo maelezo hayo yanatakiwa ili kutekeleza sheria chini ya FOIA au Sheria ya Kutoingiliwa OCR itahifadhi utambulisho wa walalamikaji kwa njia iliyo siri licha tu ikihitajika mnamo utekelezwaji wa sheria za haki za kiraia, au endapo maelezo binafsi ya mtu yanatakiwa chini ya sheria za FOIA, Sheria ya kutoingiliwa, vinginevyo maelezo binafsi ya mtu hutolewa tu chini ya misingi ya kisheria.

Chini ya Sheria ya Uhuru wa Maelezo (FOIA) anaruhusiwa afisa wa serikali kuweza kukagua faili za maelezo ya mtu zilizo katika serikali ya Shirikisho na taasisi nyingine. Maafisa waweza kupata maelezo kutoka akiba tofauti za serikali ya Shirikisho, na siyo tu vifaa vinavyo wahusu watu binafsi. OCR ni wajibu juu lake kuheshimu muongozo wa FOIA licha tu katika hali maalumu. Kwa jumla, OCR haishurutishwi kutangaza nyaraka za mlalamikaji kipindi cha utafiti wa utatuzi wa malalamiko au kipindi cha utaratibu wa utekelezaji sheria endapo kufanya hivyo ni jambo linalo weza kuzorotesha utendaji kazi wa OCR. Pia, taasisi ya Shirikisho yaweza kukataa ombi lolote la kukusanya maelezo ya mtu hata katika utekelezwaji sheria, iwapo kufanya hivyo yaweza kujiri kwamba ni ukiukwaji wa sheria ya mtu kutoingiliwa. Kadhalika, OCR yaweza kukataa kukabidhi maelezo mengine ya mtu kama vile hali ya kiafya ya mtu, iwapo kufanya hivyo ni jambo litakalo jiri kuvunja sheria ya mtu kutoingiliwa.